# MAFUA YA NDEGE



PIA, HUJULIKANA KAMA MAFUA YA AVIAN, H5N1 NA HPAI!

**Mafua ya ndege ni maambukizi ya virusi ambayo huathiri ndege lakini kwa nyakati fulani yanaweza kuambukiza binadamu na wanyama wengine. Mafua ya ndege husababisha dalili kuanzia ndogo hadi kali.**

## HALI YA SASA

**Kuna mlipuko wa mafua ya ndege nchini Marekani, na kufanya ndege walioathirika, ng'ombe wanaozalisha maziwa, na watu kuugua.**

**Hatari ya sasa kwa umma ni ndogo, lakini watu walio karibu na wanyama wenye maambukizi wako hatarini zaidi kupata maambukizi.**

**Kwa taarifa zaidi tembelea:**
**bit.ly /BirdFlu2024.**

**Maambukizi mafua ya ndege kwa binadamu hutokea hasa baada ya kuwakaribia au kugusana na wanyama wenye maambukizi bila kujikinga.**



## ZUIA MAFUA YA NDEGE

- **Epuka kukaribiana na ndege wa mwituni. Ndege kama bata mzinga na bata ni waenezaji wakuu wa mafua ya ndege, na huenda wana maambukizi hata kama hawaonekani kama wanaumwa.**
- **Waelekeze watoto wasiwaguse ndege wa mwituni au wanyama wengine, hasa katika maeneo kama vile bustani za wanyama, mashamba, na maonyesho.**
  - **Mtu yeyote anayewagusa mnyama anapaswa kunawa mikono yake kwa sabuni na maji haraka.**
- **USINYWE maziwa ghafi. Maziwa yaliyochemshwa ni salama kunywa na huua virusi vya H5N1.**

IMEREKEBISHWA MARA YA MWISHO: DESEMBA 2024

Department of Public Health
CITY OF PHILADELPHIA

## MAFUA YA NDEGE

# H5N1 KWA WATU WANAOFUGA KUKU



- Zuia ndege wako wasikutane na ndege ndege mwituni na ubadilishe maji yao angalau mara moja kwa siku.
- Tumia vifuniko na viatu vilivyopendekezwa wakati wa kuwatunza ndege zako. Badilisha nguo nguo kabla ya kuingia nyumbani kwako.
- Epuka kugusa uso wako baada ya kugusana na ndege wa mwituni au wa kufugwa au vitu ambavyo vinaweza kuchafuliwa na mate, kamasi au kinyesi. Nawa mikono yako vizuri kwa sabuni na maji.
- Fuatilia ndege wako kama wana dalili za ugonjwa na watenge ndege wowote ambao ni wagonjwa.

Toa taarifa kuhusu ndege wako wagonjwa kwenye Ofisi ya Huduma za Afya na Uchunguzi wa Magonjwa ya Wanyama ya Pennsylvania (717-772-2852, chaguo 1) na ndege wa mwituni wanaoumwa au walikufa kwenye Tume ya Uhifadhi ya Pennsylvania (833-PGC-Hunt) haraka.

Pia, unaweza kuwasiliana na daktari wa mifugo wa jimboi au USDA (866-536-7593). Pia, idara ya afya inaweza kukuomba ufuatilie dalili zako kwa siku 10 zijazo.

**CDC ina nyenzo za ziada kwa wamiliki wa mifugo: bit.ly /AvianFluCDC.**

IMEREKEBISHWA MARA YA MWISHO:
DESEMBA 2024

Department of Public Health
CITY OF PHILADELPHIA